# UKUZAJI WA MICHE YA MPENDA BURE




Septemba 2001

Kimeandikwa na

Ezekiel Kyalo & Benard Muok

## *UKUZAJI WA MICHE YA MPENDA BURE*

*Mpenda bure* ni mti wenye matumizi mengi na hutoa bidhaa nyingi tofauti kwa jamii zinazoishi sehemu kame na zisizotumika kikamilifu za kenya. ukuzaji wake umezuiwa na uchache wa miche bora. Mradi wa jamii wa ukuzaji wa misitu, kitui (SOFEM) umegundua mambo kadha yanayoweza kuendeleza ukuzaji wa mbegu za *mpenda bure* na kupuguza kutokomaa baada ya kuchipuka.

Mambo haya ni:-

- *Umri wa mbegu zilozokusanywa baada ya kukomaa.*
- *Njia mwafaka za utuzaji kabla ya kuchipuka.*
- *Wakati mwafaka wa kupandikiza miche.*
- *Uzuiaji wa miche kutokana najua, mwagaza au upepo mkali.*
- *Wakati wa kunyunyizia maji.*

## (i) Umri wa mbegu zilizokusanywa baada ya kukomaa

- Mbegu nyingi hukusanywa kutoka kwa zizi la mbuzi. Hii huakikisha ukomafu wa mbegu zilizokusanywa. Ni muhimu kuhakikisha kuwa mbegu zinazokusanywa hazijakauka (chini ya mwaka mmoja ), kwa ukuaji mwema.



**Ukusanyaji wa mbegu za *mpenda bure***

## (ii) Njia mwafaka za utunzaji kabla ya kuchipuka

Kwa ukuaji mwema mbegu za *mpenda bure* zahitaji kufanyiwa mambo yafuatayo:

1. Toa/ ondoa ganda la *Mpenda bure* ili upande mbegu iliyo ndani.



**Utoaji wa mbegu za *mpenda bure* katika kituo cha ukusaji wa miti cha Tiva kwa kutumia kifaa maalum cha kuvunjia ganda kilichotengenezwa na SOFEM/KEFRI**

2. Mbegu zilizoondolewa ukatwa kidogo ili kuendeleza uingizaji wa maji. Hili lapaswa kufanywa kwa uangalifu ili kuzuia uharibifu wa kiini cha mbegu.



*ukataji wa mbegu*

3. Baada ya kukata mbegu huwekwa kwenye maji baridi usiku kucha.



4. Shika mbegu zilizowekwa majini wima, halafu kata katikati ukitumia wembe mkali(kata kwa urefu).



*Ukataji unafanywa kwa kutumia wembe msafi na mkali*

## iii) Upanzi

Panda mbegu zilizowekwa dawa tayari kwenye masari iliyojaa changarawe na maji kwa uangalifu kabla ya kufunika kwa kutumia kartasi maalumu lililotengewa kazi hiiyo.(nailoni)



*Mbegu zilozopandwa na kufunikwa kwa kartasi maalumu ili kuifadhi hali ya juu ya joto kwenye masari ya Tiva.*

## (iv) Umri wa kupandikiza miche.

Ili kupunguza kufa kwa miche ya mpenda hure iliyo pandikizwa , ni lazima miche ipandikizwe mara tu miche inapochipuza,na kama kutacheleweshwa miche inaweza kupatwa na mstuko na mwishowe kufa.

## (v) Kufinika kuzuia kutokana na jua na mwangaza



*miche chini ya kivuli cha nyumba*

- Baada ya kuondoa miche na matawi mabaya, miche ya *mpenda bure* huhitaji karibu wiki mbili chini ya kivuli kizito



*miche iliyokingwa kutokana na mwangaza*

- Baada ya wiki mbili miche huhamishwa hadi kwenye kivuli cha mwangaza kwa karibu wiki tatu.

- Mwishoni mwa wiki hizi tatu ni salama sasa kuhamisha miche hadi sehemu iliyo wazi.



*miche kwenye sehemu wazi*

## (vi) Wakati wa kunyunyizia maji

- Miche ya *Mpenda bure* huadhiriwa na maji mengi, kwa hivyo unyunyizaji unapaswa kufanywa wakati dalili za ukavu zinapoonekana.




**KENYA FORESTRY RESEARCH INSTITUTE**
**KEFRI KITUI CENTRE**
P.O BOX 892, KITUI, KENYA
TEL:+254-141-22807/22471/22626
FAX:+254-141-22807
E-MAIL:kefrikti@wananchi.com
http://www.jicakenya.org/SOFEM/Index.htm

**KENYA FORESTRY RESEARCH INSTITUTE**
P.O.BOX 20412, NAIROBI, KENYA
TEL:+254-154-32009/32170/32891
FAX:+254-154-32009
E-MAIL:kefri@arcc.or.ke



Sanii: D. Munyao